

TANGAZO LA SERIKALI NA 624. la tarehe 01/09/2023

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,  
(SURA YA 415)

**AMRI**

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28 (3))*

AMRI YA NAULI ZA ABIRIA KATIKA NJIA YA MWANZA–BUKOBWA KATIKA ZIWA  
VICTORIA YA MWAKA 2023

SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI

- Jina                    1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Nauli za Abiria  
Katika Njia ya Mwanza–Bukoba Katika Ziwa Victoria ya Mwaka  
2023.
- Matumizi            2. Amri hii itatumiwa na Kampuni wakati ikitoa huduma  
katika njia ya Mwanza–Bukoba katika Ziwa Victoria.
- Tafsiri                3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji  
vinginevyo-
- Sura ya 415        “Sheria” maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;  
“Kampuni” maana yake ni Kampuni ya Songoro Marine  
Transport Limited iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya  
Sura ya 212        Makampuni;  
“Shirika” maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania  
lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;  
“meli” maana yake ni meli zinazoendeshwa na Kampuni katika  
Ziwa Victoria.

SEHEMU YA PILI  
NAULI NA MASHARTI YANAYOTUMIKA

- Nauli zilizoidhinishwa
4. Kampuni inayoendesha meli-
- (a) itatoza nauli kwa abiria isiyozidi viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Amri hii;
- (b) itazingatia masharti ya utoaji huduma ya usafiri kwa njia ya maji yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Majini.
- Sura ya 165
5. Wakati wa kutoa huduma, Kampuni itazingatia masharti yafuatayo:
- (a) itaweka utaratibu maalum wa utambuzi wa abiria wenye mahitaji maalum kwa kuzingatia sheria zinazosimamia masuala ya walemavu na kuwasilisha utaratibu huo kwa Shirika ndani ya miezi mitatu tangu kuanza kutumika kwa Amri hii;
- (b) itaweka utaratibu utakaowawezesha abiria wenye mahitaji maalum kusafiri bila vikwazo na kuwasilisha utaratibu huo kwa Shirika ndani ya miezi mitatu tangu kuanza kutumika kwa Amri hii;
- (c) itawasiliana na uongozi wa Bandari ya Bukoba ili kuratibu ushushaji na upakiaji salama wa abiria bila kuathiri shughuli za watumiaji wengine wa Bandari;
- (d) itabainisha katika tiketi gharama za upandaji na ushukaji wa abiria zinazotozwa na mamlaka nyinginezo, ikiwa zipo;
- (e) itaimarisha mikakati ya kimasoko ili kuongeza idadi ya abiria; na
- (f) itazingatia viwango vya usalama kama vilivyoainishwa katika Sheria ya Usafiri Majini na kanuni zake.
- Masharti ya huduma
- Sura ya 165

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(a))*

**NAULI KIKOMO ZILIZOIDHINISHWA KWA SAFARI YA MWANZA -  
BUKOBA**

<b>Daraja la Meli</b>	<b>Nauli ya Mtu Mzima (TZS)</b>	<b>Nauli ya Mtoto (TZS)</b>	<b>Nauli ya Mtu Mwenye Mahitaji Maalum (TZS)</b>
Uchumi	35,000	17,500	30,000
Biashara	50,000	22,500	40,000
La Kwanza	60,000	30,000	50,000

Dar es Salaam,  
1 Agosti, 2023

KAIMU ABDI MKEYENGE  
*Mkurugenzi Mkuu*